

SHULE YA SEKONDARI YA BWAKIRA JUU,  
S.L.P 189,  
MOROGORO,  
SIMU 0782714503  
TAREHE:.....

JINA LA MWANAFUNZI: .....

.....  
S.L.P 1880,  
MOROGORO.

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BWAKIRA JUU**

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya Bwakira juu mwaka 2021.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia 11/01/2021 hadi 18/01/2021.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**a) SARE ZA SHULE**

i. Sare ya shule hii ni shati jeupe mikono mifupi na suruali rangi ya kaki kwa wavulana na

ii. shati jeupe mikono mifupi na sketi rangi ya kaki kwa wasichana

maelezo ya mshono rinda boksi kwa wasichana na inayovuka magoti

na suruali yenye marinda mawili isiyobana kwa wavulana.

iii. Hijabu inayoruhusiwa ni nyeupe isiyokuwa na maua au urembo wowote na yenye kufunika kifua

iv. sare za michezo kwa shule hii ni .....

**b) MAHITAJI MENGINE**

i. viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba kwa wote

ii. soksi nyeupe kwa wasichana na wavulana

iii. tai ndefu kwa wote

iv. tunasisitiza suruali isibane na iwe na mkunjo chini (Turn up)

v. Daftari (counter book) tisa (9) kwa wote

vi. mkanda mweusi kwa wavulana

vii. sketi mbili n mashati mawili kwa wasichana

viii. suruali mbili na mashati mawili kwa wavulana

### 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni ( preparation) .
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sare ya shule kwa wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma

#### **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;**

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji, ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo
4. Uvutaji bangi
5. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
8. Kudharau bendera ya shule
9. Kuo au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama shule au watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kutoroka shule wakati ratiba za shule zikiendelea.

Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

- Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA BWAKIRA JUU**



**SEHEMU A (ijazwe na mzazi/ mlezi)**

Mimi ..... mzazi/ mlezi wa mwanafunzi.....

Ninaahidi kwamba nitamtunza kijana wangu ambaye ni ..... kwa kipindi chote cha masomo yake atakapokuwa shuleni na kuhakikisha kwamba mwanangu atatii na kuziheshimu sheria zote zilizowekwa shuleni vilevile nitamtekelezea mahitaji yake yote muhimu ili aweze kuendelea na masomo yake.

Sahihi ya mzazi/ mlezi.....

Jina la mzazi/mlezi.....

**SEHEMU B (ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi ... dini yangu ni..... Shule ninayotoka ..... jina la

mzazi/mlezi wa kiume ni ..... na mzazi wa kike ni

..... nikiwa kama mwanafunzi wa shule ya sekondari ya bwakira juu, ninaahidi kuwa nitazitii na kuziheshimu sheria zote za shule.

Sahihi ya mwanafunzi.....

Jina la mwanafunzi: .....

## MEDICAL EXAMINATION FORM

THE HEADMASTER  
BWAKIRA JUU SECONDARY SCHOOL,  
P.O BOX 189,  
MOROGORO.

TO BE FILLED BY MEDICAL OFFICER IN RESPECT OF ALL FORM ONE ENTRANTS

PUPIL'S NAME: .....  
AGE..... ( YEARS)  
BLOOD COUNT ( RED AND WHITE) .....  
STOOL EXAMINATION .....  
URINE ANALYSIS .....  
SYPHILIS TEST .....  
T.B TEST .....  
EARS .....  
CHEST .....  
ABDOMEN .....  
SPLEEN .....

### ADDITIONAL INFORMATION

E.g physical defects or impairments, infects chronic of family diseases Etc.

.....  
.....  
.....

I certify that above is fit/unfit for admission into a day/boarding school

Signature ..... designation .....  
Station .....  
Date .....

Note: medical officer at the time of examination please treat the individual for any illness you note. This complete form should be sent to the head of school.

No pupil or person may be enrolled without certification of physical fitness.